JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA

Dodoma,
19 Novemba, 2026

TAARIFA KWA UMMA

KUFUTA USAJILI WA KAMPUNI YA INSURANCE GROUP OF TANZANIA LIMITED

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) inautaarifa umma kuwa, kwa mujibu wa Kifungu cha 29 (b) (i) na 166 (1) (e) (ix) cha Sheria ya Bima, Sura ya 394, Toleo la mwaka 2023, imefuta cheti cha usajili wa biashara ya bima kilichotolewa kwa kampuni ya **Insurance Group of Tanzania** yenye **Na. IC20100023** kuanzia tarehe **10 Oktoba, 2026**.

Hatua hiyo inatokana na amri ya Mahakama kupitia shauri la kuifunga kampuni (Winding Up Cause No.14900 of 2029) lililofunguliwa na Kamishna wa Bima pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Divisheni ya Biashara Dar es salaam baada ya kampuni hiyo kushindwa kutimiza masharti ya utoaji wa huduma za bima kwa mujibu wa sheria.

Hivyo, umma unafahamishwa kuwa, kampuni ya **Insurance Group of Tanzania** hairuhusiwi kufanya biashara ya bima.

Mtu yeyote mwenye madai dhidi ya kampuni ya Insurance Group of Tanzania awasilishe madai yake kupitia Mfilisi wa kampuni hiyo anayepatikana kwa anuani ifuatayo:

Daniel Welwel
Asyla Attorneys
S.L.P 80496
Ghorofa ya Kwanza, Jengo la Alfa – Barabara ya *New Bagamoyo*
Dar es Salaam,Tanzania
Barua pepe: welwel@asylattorneys.co.tz
Simu: +255 786855 331

Imetolewa na

Hadija I. Maulid
Meneja Uhusiano kwa Umma na Mawasiliano
Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania